SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya kifungu cha 16(1)

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA, 2014

SEHEMU YA KWANZA

Utangulizi

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama sheria ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Msalala za Mwaka 2014, na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala.

Tafsiri

3. Katika sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo :-

“Ada na ushuru “maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala. Kwa ajili ya ada, huduma, vibali. au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.

“Afisa Muidhiniwa “maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa sheria Ndogo hizi .

“Bajaji maana yake ni chombo cha moto chenye matairi matatu na hutumika kubeba abiria au mizigo:

“Bidhaa “maana yake ni kitu chochote chenye thamani kilicholetwa sokoni au gulioni kwa lengo la kuuzwa .

“Halmashauri “ maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Msalala.

“Kibali’ maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri.

“Leseni ya biashara “maana yake ni kibali cha maandishi kinachotolewa kwa mtu binafsi, Kampuni au Taasisi kinachoruhusu kufanya biashara au shughuli yoyote katika eneo la Halmashauri.

“Machinjio “maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi

“Madini ya ujenzi“maana ni kokoto. mchanga ,na mawe

“Matangazo ya biashara“maana yake ni ishara, alama, maneno, yaliyobandikwa kwenye mabango, kuta za nyumba au vibao kwa lengo la kuitambua biashara fulani .

“Masoko“ maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kununua bidhaa:

Mkurugenzi“ maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Msalala pamoja na Afisa yeyote wa umma aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi :

SEHEMU YA PILI

UTOZAJI WA ADA NA USHURU

Ushuru 4-(1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali . leseni na huduma mbalimbali.

(2)Ada na Ushuru utozwao chini ya sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya huduma kutolewa .

(3) Ada na Ushuru utozwao kwa Halmashauri utalipwa kwa Halmashauri au wakala wake ambaye atatoa stakabadhi ya malipo yaliyofanyika.

(4) Tarehe ya mwisho ya kulipwa ushuru chini ya sheria ndogo hizi ni Tareh 25 hadi 30 ya kila mwezi .

SEHEMU YA TATU

MIPANGO MIJI

5 Ni marufuku kwa mtu yeyote :-

(a) Kuweka kontena au kujenga kibanda au jengo lolote kando ya barabara katika eneo la Halmashauri bila kupata kibali;

(b) Kubadili matumizi ya makazi kwa kuweka gereji, maegesho na matumizi mengineyo , kinyume na maombi yake kama yaliyoombwa na kuidhinishwa na Halmashauri.

6. (1) Vibanda vyote vilivyojengwa kuzunguka soko na kituo cha mabasi , vitakuwa ni Mali ya Halmashauri. Vibanda

(2) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kupangisha vibanda vyake kwa wafanya biashara watakaohitaji kufanya biashara kama inavyoelekezwa na Halmashauri .

(3) Mtu yeyote atakayepanga vyumba au vibanda vinavyozunguka soko na kituo cha mabasi , atatakiwa kujaza mkataba wa pango na Halmashauri .

(4) Endapo mpangaji atavunja mojawapo ya masharti ya upangaji wake Mkurugenzi Atatoa notisi ya kusitisha upangaji wa chumba au kibanda.

(7) Masoko yaliyoorodheshwa katika jedwali la sheria ndogo pamoja na yale yatakayoanzishwa yatakuwa ni mali ya Halmashauri. masoko

SEHEMU YA NNE

UCHIMBAJI WA MADINI YA UJENZI

8-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba au kusafirisha madini ya ujenzi bila kupata Kibali cha Halmashauri

(2) Mchimbaji au msafirishaji wa madini ya ujenzi ndani ya eneo la Halmashauri atatakiwa kulipa ada ya uchimbaji na usafirishaji madini kama itakavyooneshwa katika jedwali l

(3) Ni wajibu wa kila mchimba madini chini ya sheria Ndogo hizi, kuzingatia na Kuchukua tahadhari za athari za kimazingira zitakazotokana na uchimbaji wa madini ya ujenzi .

SEHEMU YA TANO

MATANGAZO YA BIASHARA

9- (1) Kila mfanya biashara au mtoa huduma atakayeweka mbao za matangazo au atakayetangaza biashara au huduma yake kwa kutumia vipaza sauti atatakiwa kulipa ushuru wa matangazo kwa viwango vitakavyooneshwa katika jedwali la sheria Ndogo hizi na atapewa kibali maalumu.

Ushuru wa matangazo ya biashara

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mfanyabiashara au mtoa huduma yeyote

kutumia mabango ya matangazo au matangazo ya vipaza sauti kwa nia ya kudhalilisha , kufedhehesha mtu, watu, kikundi cha watu , biashara au huduma ya mtu mwingine .

SEHEMU YA SITA

KUPIMA AFYA

10.(1) Wahudumu wote wanaohudumia biashara za vyakula na vinywaji kwenye Hoteli, Migahawa, mashine za kusaga nafaka, baa, pamoja na huduma nyingine watalazimika kupima afya pamoja na kujisajili kwa Mkurugenzi.

(2) Ada ya kupima na kuthibitishwa afya kwa mhudumu italipwa kama itavyooneshwa katika jedwali la sheria Ndogo hizi.

SEHEMU YA SABA

UTEUZI WA WAKALA

11.- (1) Halmashauri inaweza kumteua mtu binafsi, kampuni, asasi au Taasisi kukusanya ada na ushuru kwa niaba yake .

(2) wakala aliyeteuliwa chini ya sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa

(a) kukusanya na kupokea ada na ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango kilichoainishwa chini ya sheria Ndogo hizi.

(b). kuwasilisha makusanyo yote aliyowajibika kukusanya kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

(c) kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya sheria Ndogo hizi.

SHEMU YA NANE

ADHABU

. Mtu/mmiliki yeyote atakaye kataa kwa makusudi au kukwepa kulipa ada au ushuru kinyume na sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na ataadhibiwa kwa faini isiyo pungua elfu Hamsini(50000.00) na isiyozidi shilingi laki moja (100000.00) au kifungo cha muda usiozidi miezi kumi na mbili (12) au vyote viwili, faini na kifungo.

SEHEMU A

ADA YA HUDUMA YA MACHINJIO

S/NO	Mnyama	Kiasi	Idadi
1	Ng'ombe	Tsh. 5000.00	1
2	Mbuzi / Kondoo	Tsh. 1500.00	1
3	Nguruwe	Tshs. 1500.00	1

SEHEMU B

ADA YA UKAGUZI WA NYAMA

S/NO	Mnyama	Kiasi	Idadi
1	Ng'ombe	Tsh. 1500.00	1
2	Mbuzi / Kondoo	Tsh. 1000.00	1
3	Nguruwe	Tshs. 1000.00	1

SEHEMU C.

ADA NA USAJILI WA ENEO LA NGOZI

S/NO	Mnyama	USHURU	Idadi
1.	I) Ada ngozi ya ng'ombe	Tsh. 75000.00	Kwa mwezi
	II) Usajili wa eneo la ngozi		
2.	Wakubwa	Tsh. 100000.00	Kwa mwaka
	Wa kati	Tshs 50000.00	Kwa mwaka
	• Wadogo	Tshs. 20000.00	Kwa mwaka

SEHEMU D

USHURU WA KUPIMA AFYA

S/NO		USHURU	Idadi
1.	Ada ya kuandikishwa na usajili wa Mhudumu mmoja	Tshs 12000.00	Kwa mwaka
2.	Ada ya kupima Afya kwa mtu moja	Tshs. 10000.00	Kila baada ya miezi sita

SEHEMU E

USHURU WA MAZAO YA MALIASILI

S/NO	Aina ya zao	Kiasi	Idadi
1	Mkaa	Tshs. 1000.00	Kwa gunia moja
2	Vifaa vilivyotengenezwa kwa mbao a. Shata za milango b. Fremu za milango/madirisha c. Viti/stool d. Kitanda e. Seti ya kochi f. Vikapu/mikeka	 Tshs. 6000.00 Tshs. 4000.00 Tshs. 1000.00 Tshs. 6000.00 Tshs. 15000.00 Tshs. 1000.00	
3	Maombi ya Transit Pass . i) Gari chini ya Tani 7 (saba) ii) Gari zaidi ya Tani (saba)	 Tshs. 5000.00 Tshs. 10000.00	
4	Usajili wa biashara ya mazao ya misitu. i. Mbao ii. Magogo iii. Nguzo iv. Fito v. Duka bidhaa za misitu vi. Mkaa vii. Kuni viii. Furniture mart ix. Saw mill x. Fundi seremala xi. Madawa asili/kuranda/kuchana mabo xii. Mashine ya kuchakata mbao	 Tshs. 200000.00 Tshs. 200000.00 Tshs. 200000.00 Tshs. 50000.00 Tshs. 200000.00 Tshs. 200000.00 Tshs. 200000.00 Tshs. 200000.00 Tshs. 200000.00 Tshs. 400000.00 Tshs. 20000.00 Tshs. 100000.00 Tshs.200,000.00	Kwa mwaka

SEHEMU F

USHURU WA VIBAO VYA MATANGAZO

S/NO	AINA YA Tangazo	Ushuru	Ukubwa	muda
1	Matangazo yatakayobandikwa kwenye vibao na kuwekwa kando ya			

	barabara kuu (a) Yasiyotoa mwanga (b) Yanayotoa mwanga	Tsh. 3000.00 Tsh. 5000.00	Kila ft1 ya mraba Kila ft 1 ya mraba	Kwa mwaka Kwa mwaka
2	Matangazo ya biashara yanayobandikwa kwenye nyumba ya biashara (a) Yasiyotoa mwanga (b) Yanayotoa mwanga	Tsh. 2000.00 Tsh. 2500.00	Kila ft. 1ya mraba Kila ft. ya mraba	Kwa mwaka Kwa mwaka
3	Matangazo ya biashara yatakayobandikwa kwenye nyumba za makazi	Tsh. 1000.00	Kila ft 1 ya mraba	Kwa mwaka
4	Matangazo ya biashara kwa njia ya kipaza sauti	Tsh.10000.00	Kwa siku moja	Kwa siku

SEHEMU G

ADA YA USAJILI WA MAGARI YA BIASHARA NA MIZIGO

S/No.	Aina ya gari	Ada	Muda
1.	Taxi	Tsh. 40000.00	Kwa mwaka
2.	Pick Ups	Tsh. 50000.00	Kwa mwaka
3.	Trekta	Tsh. 60000.00	Kwa mwaka
4.	Lori za biashara 3.5 toni-10 toni	Tsh. 70000.00	Kwa mwaka
5.	Lori za Biashara 11 toni na kuendea	Tsh. 100000.00	Kwa mwaka

SEHEMU H

ADA YA KUCHANGIA UPIMAJI WA VIWANJA

S/NO	Aina ya uwanja	Ada
1	Kiwanja kidogo (high Density)	Tsh . 100000.00
2	Kiwanja cha kati (Medium Density)	Tsh. 150000.00
3	Kiwanja kikubwa (low density)	Tsh. 200000.00
4	Kiwanja kikubwa zaidi (super low Density)	Tsh. 250000.00

SEHEMU I

KIBALI CHA UJENZI

S/NO	Aina ya jengo	Ushuru
1.	Ghorofa 1	Tsh . 120000.00
2.	Ghorofa 2 na kuendelea	Tsh. 150000.00
3.	Nyumba za biashara	Tsh. 100000.00
4.	Ghala au bohari	Tsh. 200000.00
5.	Kituo vya mafuta	Tsh. 250000.00
6.	Nyumba za makazi	Tsh. 30000.00
7.	Nyumba za makazi na biashara	Tsh. 70000.00
8.	Majengo mengine ambayo hayakutajwa hapo juu	Itategemea aina ya jingo
9.	Minara	1000000.00

SEHEMU J

ADA YA MABADILIKO YA JENGO LILILOPO (ALTERATION)

S/NO	Aina ya nyumba	Ushuru
1.	Nyumba ya makazi	Tsh. 2000.00
2.	Nyumba ya biashara	Tsh. 50000.00
3.	Nyumba ya Ghorofa	Tsh. 200000.00
4.	Kiwanja , bohari, ghala	Tsh. 100 000.00
5.	Jingo lolote ambalo halijatajwa	Itategemea aina ya jengo

SEHEMU L

ADA YA KUMILIKI SILAHA

S/NO	Aina ya ada	Kiwango
1.	Kumiliki Silaha (Gobore)	Tsh. 5000.00 kwa mwaka

SEHEMU M

USHURU WA MADINI YA UJENZI

S/NO	AINA YA MADINI	USHURU	UJAZO
1.	CHANGARAWE / KOKOTO /MAWE/ KIFUSI	Tsh. 500.00 kwa kila tani inayochimbwa au kusafirishwa	

SEHEMU N

KODI YA PANGO MAJENGO NA VIBANBA VYA HALMASHAURI

S/.No	Aina ya jengo	Kodi ya pango	Muda
1.	Vibanda ndani ya soko	Tsh. 10000.00	Kwa mwezi
2.	Vibanda nje ya soko	Tsh. 10000.00	Kwa mwezi
3.	Vibanda ndani ya stendi	Ths. 10000.00	Kwa mwezi
4.	Vibanda nje ya stendi	Tsh. 10000.00	Kwa mwezi
5.	Nyumba ya makazi ya Halmashauri (a) Nyumba	Tsh. 10000.00	Kwa kila mpangaji

SEHEMU O

MAJENGO YA HALMASHAURI YALIYOKO SOKO KUU

S/NO	AINA YA JENGO	USHURU
1.	Mabucha	Tshs 40000.00 kwa mwezi
2.	Maduka makubwa	Tshs. 50000.00 kwa mwezi
3.	Vibanda vipya 12 @ meza 8	Tshs. 5000.00 kila meza kwa mwezi
4.	Meza 45 zilizo katikati ndani ya soko kuu	Tshs. 5000.00 kwa meza kwa mwezi

SEHEMU N

VYOO

S/NO	AINA YA JENGO	USHURU
1.	Choo cha soko kuu-Bugar.	200.00 kwa kila kichwa
2.	Choo Bulige	200.00 kwa kila kichwa

SEHEMU P

USHURU WA MAZAO MCHANGANYIKO

S/NO	AINA YA ZAO	USHURU
1.	Mahindi	Tshs. 1000.00 kwa gunia
2.	Mchele/mpunga	Tshs 1000.00 kwa gunia
3.	Maharage	Tshs 1000.00 kwa gunia
4.	Karanga	Tshs 1000.00 kwa gunia
5.	Alizeti	3% ya bei ya kununulia
6.	Miwa	3% ya bei ya kununulia
7.	Pamba	10% ya bei ya kununulia
8.	Dengu	Tshs.1000.00 kwa gunia
9.	Mazao mengine ambayo Hayakutajwa	3% ya bei ya kununulia

SEHEMU Q

USHURU WA MASOKO/ GULIO

S/No	Aina ya bidhaa	Ushuru	Muda
1.	Nguo za mitumba	Tsh. 1000.00	Kwa siku
2.	Nafaka rejareja	Tsh. 1000.00	Kwa siku
3.	Madawa asili	Tsh. 1000.00	Kwa siku
4.	Migahawa ndani ya soko	Tsh. 1000.00	Kwa siku
5.	Samaki rejareja	Tsh. 1000.00	Kwa siku
6.	Mboga za majani	Tsh. 1000.00	Kwa siku
7.	Dagaa rejareja	Tsh. 1000.00	Kwa siku
8.	Wauza vyungu	Tsh. 1000.00	Kwa siku
9.	Miwa rejareja	Tsh. 1000.00	Kwa siku
10.	Matunda/ nyanya/ vitunguu	Tsh. 1000.00	Kwa siku
11.	Viatu rejareja	Tsh. 1000.00	Kwa siku
12.	Bidhaa nyinginezo	Tsh. 1000.00	Kwa siku
13.	Bidhaa zote zikiwemo za kilimo siku ya gulio zitatozwa	Tsh. 1000.00	Kwa siku ya gulio tu

SEHEMU R

USHURU WA MINADA

S/NO	AINA YA MNYAMA	USHURU	IDADI
1	Ng'ombe	Tsh. 5000.00	Kwa kila Ng'ombe
2	Mbuzi /Kondoo	Tsh. 1500.00	Kwa kila mbuzi /kondoo
3	Nguruwe	Tsh. 1500.00	Kwa kila Nguruwe

SEHEMU S

USHURU WA STAND NA MAEGESHO

S/NO	AINA YA GARI	USHURU	IDADI
1.	Mabasi /malori	Tsh. 2000.00	Kwa siku
2.	Hice	Tsh. 1000.00	Kwa siku
3.	Taxi	Tsh. 500.00	Kwa siku
4.	Bajaji	Tsh. 500.00	Kwa siku

II. MAEGESHO

S/NO	AINA YA GARI	USHURU	IDADI
1.	Lori/mabasi	Tsh. 2000.00	Kwa siku
2.	Hiace	Tsh. 1000.00	Kwa siku
3.	Taxi	Tsh . 500.00	Kwa siku
4.	Bajaji/Pikipiki	Tsh. 500.00	Kwa siku
5.	Magari watu binafsi	Tshs. 500.00	Kwa siku

SEHEMU T

USHURU WA NYUMBA ZA KULALA WAGENI

S/NO	AINA YA GESTI	USHURU	IDADI
1		Asilimia 20% kwa kila kitanda	Kwa siku

SEHEMU U

LESENI YA VILEO

S/NO		USHURU	IDADI
1.	Wauzaji wa jumla	Tshs. 60000.00	Kwa mwaka
2.	Baa	Tshs. 40000.00	Kwa mwaka
3.	Grocery	Tshs. 30000.00	Kwa mwaka

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe…… Mwezi……..…,2014 na Kubandikwa mbele ya:

PATRICK KARANGWA

Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya ya Msalala

MIBAKO MABUBU,

Mwenyekiti

Halmashauri ya Wilaya ya Msalala

NAKUBALI,

Dodoma

Tarehe……..2014

MHE. MIZENGO PETER PINDA (MB.)

Waziri Mkuu